**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 1 No. 1 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i1.94


# Mabadiliko Kimaana na Kimatumizi katika Methali za Kijinsia: Mifano kutoka Jamii ya Wanyankole

**Annensia Arinaitwe, Mosol Kandagor & Magdaline Wafula**
*Chuo Kikuu cha Moi*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa 2023-03-14*
*Rekebishwa 2023-04-28*
*Kubalika 2023-05-18*
*Chapishwa 2023-05-19*

***Maneno Muhimu***
Jinsia
Kinyankole
Maana
Mabadiliko

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Annensia Arinaitwe, A., Kandagor, M. & Wafula, M. (2023). Mabadiliko Kimaana na Kimatumizi katika Methali za Kijinsia: Mifano kutoka Jamii ya Wanyankole. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *1*(1), Ku. 1-8.
*Copyright © 2023 The Author*
CC BY

**Ikisiri**
Makala hii inachunguza mabadiliko kimaana na kimatumizi katika methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole. Lengo kuu la makala hii ni kubainisha athari ya mabadiliko katika jamii kwa kujikita kwenye ufasiri wa maana na matumizi ya methali za kijinsia miongoni mwa Wanyankole nchini Uganda. Mbinu za mahojiano zilitumika katika ukusanyaji wa data. Utafiti huu ulihusisha methali kumi na tano za kijinsia katika jamii ya Wanyankole. Uteuzi huo ulifanyika kimaksudi kwa kuwa utafiti ulilenga kuchanganua methali zilizohusu jinsia za kike na kiume katika jamii ya Wanyankole. Nadharia ya Udenguzi ilitumika katika uchanganuzi wa data. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa kadri ulimwengu unavyobadilika ndivyo jamii ya Wanyankole inavyobadilika. Hivyo basi mabadiliko haya yameathiri ufasiri wa maana na matumizi katika methali za kijinsia za Wanyankole. Makala hii inapendekeza kuwa baadhi ya methali zinafaa kuchunguzwa upya kiufasiri, kimuundo na kimatumizi ili uamilifu wake uwiane na jamii ya kisasa.

## Utangulizi

Methali ni kipera cha fasihi simulizi ambacho hutumika kuwafanya watu katika jamii kutafakari, kupima maisha, kuelimika na kuweka mikabala itakayodhibiti mustakabali wao. Jamii ya Wanyankole miongoni mwa jamii nyingine duniani, ina shehena kubwa ya kipera hiki cha fasihi simulizi na hasa methali za kijinsia ambazo zimetumika tangu katika jamii katika hii. Methali hizi

zimekuwa zikitumika katika mazungumzo tangu hapo jadi hadi leo. Methali za kijinsia zimeenziwa sana katika jamii ya Wanyankole kwa sababu zimechangia pakubwa katika kutengea kila jinsia majukumu yake kuliko kipera kingine chochote cha fasihi. Kwa muda mrefu methali za kijinsia zimekuwa zikitumika kuielimisha jamii ya Wanyankole katika miktadha tofauti tofauti kama vile: ndoa, elimu, siasa, uchumi na dini. Wanajamii walichangamkia majukumu yao bila pingamizi zozote hadi karne ya ishirini na kuendelea. Katika kipindi hiki, mambo yalianza kubadilika kutokana na vuvumuko la usawa wa kijinsia lilipopamba moto kutokana na fursa ya jinsia zote kupata elimu shuleni na kuanza kudai kushiriki kikamilifu katika nyanja mbalimbali za maisha.

Ni kutokana na mtazamo huu, ndipo makala hii imetazama upya methali husika za kijinsia katika jamii ya Wanyankole. Hali hii imechochewa na wazo kuwa, kadri ulimwengu unavyobadilika, ndivyo jamii ya Wanyankole vilevile inabadilika. Hii ina maana kuwa maoni ya vijana na wasomi yamkini ni tofauti na yale ya kina babu walipokuwa wakitunga methali hizi za kijinsia. Kwa hivyo ili kuweza kutambua mitazamo hiyo tofauti, makala hii inachunguza methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole huku ikitathmini mabadiliko kimaana na kimatumizi kutoka jamii ya jadi hadi jamii ya kisasa. Aidha, makala hii inapambanua sababu za kutokea kwa mabadiliko hayo katika jamii ya Wanyankole.

**Dhana ya Jinsia katika Jamii ya Wanyankole**

Jamii ya Wanyankole ni mojawapo ya jamii ambayo inapatikana magharibi mwa Uganda. Jamii hii hutumia lugha yao asilia ambayo ni Runyankole katika shughuli za kila siku na ambayo ni mojawapo ya lugha za kibantu. Mohammed (2000) na Iribe na Mukhwana (2011) wanadai kuwa jinsia ni kigezo cha maumbile ambapo kibayolojia kinadhihirisha iwapo mtu anayezungumziwa alizaliwa akiwa mke au mume, pamoja na majukumu yanayohusishwa na maumbile hayo. Katika jamii ya Wanyankole wanaume hutengewa majukumu na hupewa hadhi tofauti na wanawake. Hali hii hujitokeza katika methali nyingi za kijinsia. Kwa mfano mwanamume huchukuliwa kuwa na uwezo wa kila kitu na maneno yake ni lazima yawe ya kuamrisha ili atambulike kuwa ni mwanaume kamili. Hali hii inadhihirika katika methali nyingi za Wanyankole. Mathalani katika methali hii; "*Omushaija aba byoona*" (mwanaume ndiye kila kitu) ni bayana kuwa mwanamume amepewa hadhi ya juu zaidi akilinganishwa na mwanamke katika jamii ya Wanyankole. Hivyo basi, dhana jinsia katika makala hii inahusu majukumu au hadhi ambayo huhusishwa na mwanamke au mwanamume katika jamii ya Wanyankole.

Makala hii imeegemezwa kwenye nadharia ya Udenguzi kwa sababu ilinuia kutathmini jinsi mabadiliko katika jamii ya kisasa yamekiuka ufasiri wa maana katika methali za kijinsia miongoni mwa jamii ya Wanyankole. Udenguzi ni nadharia iliyoasisiwa na Mfaransa Jacques Derrida (1967). Derrida (*keshatajwa)* alianza kutumia neno '*deconstruction*' alipokuwa akijadili athari za kuelewa lugha kama maandishi bali si usemi. Derrida (1976) anaendelea kudai kuwa, mtazamo ambao umekubalika kuhusu ulimwengu na lugha ukichunguzwa kwa kuangazia matumizi ya ishara tunazozifahamu, taswira itakayojitokeza ni tofauti na ile tunayoifahamu. Derrida anaeleza zaidi kuwa udenguzi huhusu ukinzani wa jozi za maneno. Derrida (1976:50) anasema hivi:

> "Kusoma kwa makini kwa matini huleta vinyume ambavyo havina mwisho. Hata hivyo, msomaji hatakiwi kukoma bali anapaswa kuendelea kusoma na kung'amua vinyume vingi kadri ya uwezo wake. Aidha kile kinachorejelewa huwa ni ishara ambayo aghalabu huendelea kubadilika na kuwa kitu


2

> kingine, yaani kinachorejelewa pia hurejelea kitu kingine na azimio la udenguzi ni kuianisha matini kwa njia ya kisanaa ili kuonyesha kile hakifahamiki" *(Tasfiri yangu).*

Kwa hivyo, nadharia ya udenguzi huzama katika ufafanuzi wa matini na kuyatazama kwa jicho la ndani kwa kuyadengua na kuyabomoa ili kubaini maana mbadala. Nadharia hii inadai kuwa uelewaji wa ndani wa matini unaweza kutupa mwanga kamili kuhusu jamii husika. Kwa msingi huu, uchunguzi wa methali za kijinsia kiudenguzi unaweza kutupa mwanaga kuhusu maendeleo ya jamii ya Wanyankole kijamii, kisiasa na hata kiuchumi.

Mwamzandi (2013) anabainisha kuwa mbinu kuu na muhimu inayotumiwa na wanaudenguzi ni ukinzani wa jozi za maneno. Kwa hivyo, kwa kutumia nadharia ya udenguzi katika uchanganuzi wa methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole, tulibainisha methali za kijinsia na kuzifafanua ili kupata maana na matumizi ya methali husika katika miktadha tofauti kwa kulinganisha jamii ya kijadi na ile ya kisasa.

Schmitz (2007) anaeleza kwamba wanaudenguzi husisitiza kufuatilia maana ya maneno kama inavyotarajia zoezi la kidenguzi ili kubainisha kile kisicho na athari yake katika uwanja mzima wa maana. Kulingana na Schmitz, ni kutokana na maneno kwenye matini ambapo tunaweza kufanya udenguzi ili kupata kwa kweli maana iliyokusudiwa. Ubomozi huu wa kazi hufanyika ili kuweza kupata dhana mpya kabisa kwa wasomaji wa kazi husika. Mawazo haya yanawiana kwa kiasi na ya Carter (2006) anayedai kuwa watu hupania tu kuweka mipaka kati ya vitu vya kufikirika na udenguzi kwa upande mwingine hutuelekeza katika kuchunguza kwa makini ukinzani unaojitokeza ndani ya matini. Kwa maoni ya Carter, tunaweza kupata maana tofauti ya matini yenyewe na kwa hivyo tukabomoa mipaka na imani tuliyokuwa nayo kuhusiana na matini hiyo.

Miller (1976) anasema kuwa udenguzi ni juhudi ya kufikia nguvu na uwezo wa matini kama chombo kinachoweza kujifafanua. Anaendelea kusema kuwa matini ni kazi ambayo inaweza kujieleza na kujifafanua kwa mapana. Kwa mfano, methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole zinaposomwa tena, mawazo mapya ambayo hayakuibuliwa awali yanaweza kuchipuka kwa kuelekezwa na nadharia ya Udenguzi. Hii ni kwa sababu usomaji wa matini yoyote huathiriwa kwa kiasi kikubwa na muktadha mahsusi.

Kwa jumla, udenguzi unachunguza lugha kama chombo cha mawasiliano yenye utata, na uwezo wa kujifafanua, hasa katika maandishi. Ni uchambuzi unaoweka wazi ukinzani wa fasihi na matini nyingine zisizo za kifasihi. Nadharia ya udenguzi inapinga mgao mkali wa hali mbili au zaidi zinazokinzana, na kuonyesha uwezekano wa hali kama hizo kuwa pamoja na kuchangiana kimaana. Tuliongozwa na mihimili mahsusi ya nadharia ya Udenguzi katika uchanganuzi wa kipragmatiki wa methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole.Nadharia ya udenguzi ina mihimili ifuatayo kwa mujibu wa Rorty (1996), Mohamed (2006), pamoja na Wafula na Njogu (2007):

i. Udenguzi ni ukiushi wa kaida za matini.
ii. Hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Hii ndiyo inayowafanya wahakiki kutoa fasili tofauti tofauti kuhusu dhana moja. Fasili hizo zaweza kufanana au kutofautiana. Kwa hiyo, udenguzi unaweza kuboresha matini au kuumba upya kwa lengo la kukidhi upya mahitaji ya jamii.
iii. Msomaji wa matini fulani anaweza kimakusudi kupoteza maana kabisa kwa vivuli vya maana.


3

iv. Nadharia ya udenguzi hulenga kufutilia mbali mipaka katika jozi za maneno; kuwa ni mfano wa sarafu moja yenye pande mbili.
v. Udenguzi hushughulikia maneno yanayokinzana na wakati huo huo kubainisha itikadi kuu inayojitokeza na inayostahili kusailiwa upya.
vi. Udenguzi ni uhakiki unaokita na kuzingatia matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha.

Msingi wa data katika utafiti huu ulikuwa ni methali zilizoteuliwa kimaksudi kutoka jamii ya Wanyankole. Utafiti huu ulihusisha methali kumi na tano za kijinsia katika jamii ya Wanyankole. Uteuzi huo ulifanywa kimaksudi kwa sababu utafiti ulilenga kuchanganua methali zilizohusu jinsia za kike na kiume katika jamii ya Wanyankole. Mbinu ya mahojiano ilitumiwa kukusanya data kutoka kwa wasailiwa kumi na wawili kule nyanjani. Data iliyokusanywa ilianishwa kwenye makundi mawili makuu; kundi la wahojiwa wa umri kati ya miaka 25-45 waliowalisha jamii ya kisasa na vilevile wahojiwa wenye umri kati ya miaka 50-80 waliowakilisha jamii ya jadi ya Wanyankole. Isitoshe, katika makundi haya mawili, methali husika za kijinsia ziligawanywa katika makundi mawili: Methali za kijinsia zilizohusu wanawake na zile zilizohusu wanaumme.

**Matokeo ya Utafiti**

Katika sehemu inayofuata, tumeangazia matokeo kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Tumejikita hasa kwenye maana na matumizi yake hasa katika methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwenye nyanja mbalimbali za maisha yao.

**Maana na Matumizi ya Methali za Kijinsa katika Jamii ya Wanyankole**

Utafiti huu ulichunguza methali za kijinsia za Wanyankole zilivyojitokeza kimaana na kimatumizi katika miktadha tofauti kama vile: elimu, ndoa, madili na malezi, tamaduni, kazi, dini, siasa na uchumi kwa kutumia kipengele cha kipragmatiki. Kisha kutathmini iwapo pana mabadiliko ya kimaana na kimatumizi baina ya jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole. Kwa kufanya hivi, makala hii iliweza kupendekeza ni methali zipi zilizohitaji kubadilishwa, kuondolewa na kuhifadhiwa namna zilivyo katika jamii husika.

**Ndoa**

Katika utamaduni wa Wanyankole, ndoa ni suala ambalo lilikuwa nguzo kuu katika familia na hata jamii kwa jumla. Ni jambo ambalo liliheshimiwa sana na kila mtu, na ilikuwa lazima msichana alipohitimu miaka kumi na minane wazazi wake wamwoze. Mtoto wa kike hakuruhusiwa kurandaranda kijijini. Naye mtoto wa kiume alipaswa kuoa alipohitimu umri wa miaka kumi na tisa ili kuthibitisha kuwa amekuwa mtu mzima. Alistahili kufanya kazi kwa bidii ili aweze kupata ng'ombe wa kutoa mahari kwa wakwe zake. Ingawa jinsia zote mbili zilitarajiwa kuolewa na kuoa, methali zilizotumiwa zilionyesha ujinsia katika kila shughulizilizopatikana katika ya jamii ya Wanyankole. Kila mtu alikuwa alitengewa kazi na nafasi maalum katika jamii. Kwa mfano, mwanamke alikuwa na jukumu la kuzaa na kulea watoto, kumfurahisha mumewe kingono, kupika, na kuhakikisha usafi wa nyumbani unadumishwa. Naye mwanamume alikuwa na jukumu la kulinda familia yake, kuwinda, kuhudhuria mikutano, kujenga nyumba, kukama na kuwapeleka ngo'mbe zizini, kuchinja wanyama na kuleta vyakula nyumbani. Kwa hivyo jamii hii ilikuwa na mila, desturi na utamaduni wake ambao ilijivunia sawa na jamii nyinginezo ulimwenguni.

Katika uchanganuzi wa methali kumi na tano za kijinsia, mtafiti aligundua kuwa methali zote zilizokuwa zimeteuliwa zilikuwa zinazungukia suala kuu la ndoa. Hivyo mtafiti aliteua vijipengele


4

Vol. 1 No. 1 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i1.94


vingine vidogo vidogo ndani ya mada kuu ya ndoa, ili kuonyesha vilivyojitokeza katika miktadha tofauti ya jamii kama vile; malezi na maadili, utamaduni, kazi, uchumi, siasa, dini na elimu.

**Ndoa na Maadili**

1. Kinyankole: Omukaziotamanyire *ekimutungire eyaiba agikwatisa omukono gumwe*.

   Kiswahili: Mwanamke asiyejua linalomtunza hushika ume wa mumewe kwa mkono mmoja.

Methali **1** hapo juu ilieleweka kimuktadha kuangazia suala la ndoa. Kimsingi methali hii ilimaanisha mwanamke yeyote aliyekosa kujua umuhimu wa mumewe alimdharau kwa kutompokea kwa heshima. Katika jamii ya jadi ya Wanyankole, kina babu walitumia methali hii kuwaonya wanawake wasije wakawapuuza waume zao. Mwanamke alipaswa kumheshimu mumewe kwa sababu alikuwa amemtolea mahari alipomtoa kwao na kutwaa jukumu la kumtunza yeye na wanawe. Kwa hivyo alifaa kushukuru kwa kutunikiwa mume na mlinzi na kwa hivyo alifaa kumtumikia kikamilifu kwa heshima. Kwa msingi huu, methali **1** ilikuwa na ufaafu katika jamii ya kijadi kwa sababu ilikuwa inamkumbusha mwanamke jukumu lake la kumtii mume kwa kuwa ndiye aliyeonekana kuwajibikia familia yake enzi hizo. Hata hivyo methali hii imeathirika kimkutadha, kimaana na kimatumizi kutokana na mwamko mpya katika jamii ya kisasa kwa upande wa uchumi, siasa, utamaduni, elimu na ndoa. Mabadiliko haya yamechochea ushirikiano baina ya mwanamke na mwanamume ili kuchapuza maendeleo katika jamii za kisasa. Kwa msingi huu, suala la heshima na uwajibikaji wa kifamilia linahusisha jinsia zote mbili na wala si jukumu la mwanamume pekee ilivyokuwa haoa awali.

**2**. Kinyankole: *Omwana mubi ajumisa nyina.*

Kiswahili: Mtoto mbaya husababisha mama yake kutukanwa.

Katika jamii ya jadi ya Wanyankole, ilitambulika katika muktadha wa ndoa kuwa mama alikuwa ametengewa jukumu la ulezi. Hili lilitokana na na maumbile yake na uhusiano aliokuwa nao na watoto tofauti na mwanamume. Kwa msingi huu, jamii ilimtegemea kuzaa na kuwalea hao watoto vizuri. Mtoto alipokwenda kinyume na matarajio ya jamii, mama ndiye alilaumiwa. Hata hivyo, katika muktadha wa kisasa mambo yamebadilika. Kwa sasa jinsia zote zinatekeleza kazi sawa. Hivyo, hakuna muda mwingi wa mama kuwa na watoto. Yaani, mara nyingi watoto huwa shuleni, hivyo muda wao nyumbani umepunguka mno. Kwa msingi huu, methali hii inahitaji kudenguliwa kimaana na kimatumizi.

**3.** Kinyankole: *(Emboko) Ezi waterwa nyoko tiziba nkoni.*

Kiswahili: (Viboko) ulivyochapwa na mama yako si viboko.

Methali hii ilidhihirisha kwamba mama alikuwa na uwezo wa kuadhibu mtoto alipokosa bila kulaumiwa na mtu yeyote katika jamii. Katika utamaduni wa Wanyankole mwanamke alikuwa nguzo kuu katika malezi ya watoto. Hii ni kwa sababu mama alikuwa na uhusiano wa karibu sana na watoto tukilinganisha na baba. Kwa hivyo mama alipomuadhibu mtoto iliaminiwa kuwa alifanya hivyo kwa nia ya kumkosoa na wala si kumdhuru.

**Ndoa na Urithi**


5

**4.** Kinyankole: *Omukazi ayomba azibira Omutabani kuragwa.*

Kiswahili: Mwanamke mgomvi huzuia mtoto wake wa kiume kurithishwa.

Jamii ya Wanyankole imejengeka kwenye mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa msingi wa ubabe-dume. Kutokana na msingi huu, lilikuwa ni jambo la muhimu mwanamume kuwa na mrithi ili kuendeleza kizazi chake. Hii ilimaanisha kuwa mwanamume aliyekuwa anajiandaa kuoa ilibidi amtafute mwanamke mwenye sifa nzuri za kumwezesha mtoto wake wa kiume kurithishwa. Sifa ambazo jamii ilitazamia zilikuwa: mwanamke mpole, mvumilivu, mkarimu, mwenye bidii, mwenye upendo na huruma. Ikiwa mwanamke alikuwa hana sifa hizo, iliaminiwa kuwa hangeweza kuwalea watoto na hasa wa kiume vizuri na hivyo kutishia mumewe kutokuwa na mrithi. Madai ya methali **4** yanapingwa na jamii ya kisasa kutokana na mabadiliko aa Wanyankole. Jinsia zote siku hizi zina jukumu la kulea watoto na suala la maadili linahusisha jinsia zote na wala si mwanamke tu.

**Ndoa na Utamaduni**

**5.** Kinyankole: *Omukazi taba mugyeni.*

Kiswahili: Mwanamke hawi mgeni.

Kitamaduni mwanamke Mnyankole hakustahili kupumzika. Madai yakiwa, kutoka utotoni alikuwa amefunzwa kufanya kazi bila kuchoka tofauti na jinsia ya kiume. Kutoka utotoni jinsia hizi mbili zilifunzwa kazi tofauti, mfano mwanamke alifunzwa kupika, kuzaa na kulea, kumfurahisha mwanaume kingono na kuhakikisha usafi nyumbani. Kwa upande mwingine, mwanamume alifunzwa kuwa mwindaji hodari, mjenzi, hakimu na mlinzi wa usalama. Kwa hivyo kitamaduni, mwanamke hakustahili kuwa mvivu hasa kuhusiana na kazi za nyumbani. Lakini katika jamii ya kisasa, kuna mtazamo tofauti kutokana na mwamko mpya unaochochewa na mabadiliko katika uchumi, siasa, elimu, utamaduni na ndoa. Mwanamke wa kisasa hajishughulishi na shughuli za nyumbani tu hali kadhalika mwanamume wa kisasa. Leo hii tuna wanawake Wanyankole ambao wanajishughulisha na masuala ya uongozi na ulinzi wa nchi kama askari ilhali kuna wanaume Wanyankole ambao ni wapishi Hodari katika hoteli za kitafa na kimataifa. Kwa hivyo, uamilifu wa methali hii unaelekea kudidimia kadiri wakati unapita.

**6**. Kinyankole: *Omukazi oine iba tarya nkoko.*

Kiswahili: Mwanamke aliye na mume hali kuku.

Kutokana na ufasiri wa kizazi kizee wa methali **6** hapo juu, ni wazi kuwa kitamaduni mwanamke hakustahili kula nyama ya kuku kwa madai kuwa ni wanaume ambao walikwa wanafanya kazi ngumu na walistahili kula vizuri ili kupata nguvu ya kufanya majukumu mengi katika jamii. Hii inamaanisha kuwa utamaduni ulikuwa umemnyima mwanamke uhuru wa 'kula vizuri' kwa madai kuwa alikuwa mtu dhaifu. Kutokana na madai haya, jamii ya kisasa imelazimika kupinga methali hii kwa madai kuwa imepitwa na wakati. Katika jamii ya kisasa, jinsia zote zinahitaji lishe bora ili kushirikiana kikamilifu katika maendeleo ya jamii yao. Mfumo-dume wa jamii ya jadi ulielekea kuipendelea jinsia ya kiume katika masuala ya lishe bora hali inayopingwa na kizazi cha sasa.

**Ndoa na Malezi**

**7.** Kinyankole: *Enaku y'otangabire nyoko tetuba.*


6

Kiswahili: Tatizo ambalo hujamwambia mamako halipungui.

Kimaana na kimatumizi methali hii ilirejelea jukumu la mama katika malezi kwenye jamii. Katika jamii ya Wanyankole mwanamke alikuwa na wajibu muhimu wa kuzaa na kuwalea watoto katika muktadha wa ndoa. Majukumu yaligawanywa kati ya mwanamume na mwanamke na kila mtu alikuwa lazima awajibike katika kazi yake. Kwa mfano; mwanamumme alistahili kuwa kiongozi na kuwajibikia familia yake. Mwanamke alistahili kuzaa watoto, kuwalea, kuwapikia na kudumisha usafi nyumbani. Kutokana na malezi mazuri ya mama, watoto walipata uhuru wa kumwambia lolote lililokuwa linawakera moyoni tofauti na baba. Mama alitazamiwa kuwa mtu mwenye sifa za upole, ukarimu, mvumilivu na mwenye upendo tukimlinganisha na baba. Kutokana na sifa hizi, mama alipewa jukumu la malezi ya watoto.

Ijapokuwa katika jamii ya jadi jukumu la malezi na maadili ya Watoto lilitengewa hasa mama mzazi, katika jamii ya kisasa, baba na wakashikadau wengine kama vile walimu katika taasisi za elimu na viongozi wa dini wanapaswa kushirikiana katika malezi ya kizazi kichanga. Kwa msingi huu, methali hii inahitaji kufasiriwa upya ili iafikiane na hali halisi ya jamii ya kisasa ya Wanyankole.

**Hitimisho**

Kutokana na makala hii imebainika kuwa suala la jinsia limejitokeza mno katika methali za Wanyankole. Mada kuu zinazotawala katika methali hizi ni ndoa na utamaduni, ndoa na maadili, ndoa na malezi, ndoa na urithi miongoni mwa mengine. Makala hii vilevile imedhihirisha kwamba utamaduni ulichangia pakubwa katika kuleta ujinsia katika jamii hii pale ambapo mwanamke hakuweza kujikomboa. Isitoshe hata ikiwa kipengele cha utamaduni kilikuwa na methali nyingi si kwamba zote zilikubaliwa katika jamii ya kisasa. Kuna baadhi ya methali ambazo zimeondolewa na zingine zinahitaji kuchunguzwa tena kikamilifu ili kubainisha nafasi zao katika jamii. Vilevile methali zilizohusu ndoa na maadili zilijadiliwa na kupendekezwa kuwa, baadhi ya methali hizi zibadilishwe kutokana na mabadiliko ya kimaana yanayochochewa na mabadiliko katika jamii. Hali hii imechangiwa na hoja kuwa kadri ulimwengu unavyobadilika ndivyo jamii ya Wanyankole inavyobadilika. Hivyo basi mabadiliko haya huathiri mfumo mzima wa jamii ikiwemo fasihi.

## Marejeleo

Chafetz, J. (1974). *Masculine / Feminine or Human?* Itasca, IL: Peacock Publishers. Fetter lane.

Derrida, J. (1976). Freud und der Schauplatz der Schrift. *Die Schrift und die Differenz*.

Finnegan, R. (1992). *Oral Tradition & Verbal Arts*. London: Routledge press, New Gokumanya Publishers.

Iribe, M. P. I. na Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii.* Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Izugbara, C. O. (2005). "Hypothesis on the Origin of Hegemonic Masculinity" *In Sexuality in African Magazine.* Lagos Africa Regional Sexuality Resource Centre 2(1), pp. 13-14.

Kibigo, M. L. (2019). *Ubabedume katika Majigambo ya Miviga ya Shilembe na Mchezasili wa Mayo ya Waisukha Nchini Kenya kwa Mtazamo wa Kisemantiki. (*Tasnifu ya Uzamifu ambayo imewasilishwa kwa East African Journal of Swahili Studies, 4(1), 2019.

Kibigo, M. L., Choge, S. C., & Simiyu, F. W. (2019). Tamathali za Semi Zinazosawiri Ubabedume katika Majjigambo ya Miviga ya Shilembe na Mchezasili wa *Mayo* ya Waisukha, Nchini Kenya kwa Mtazamo wa Semantiki. Tasnifu ya Uzamifu iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia.

Maingi, R., (2005). The Kenyan Constitutional Reforms Process: A Case Study on the Work of PIDA Kenya in Securing Womens Right. *Feminist Africa* .

Mwamzandi, I. (2013). Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia za Fasihi. In *Swahili forum* (Vol. 20)

Ruether, R. (1974). *Religion and Sexism.* New York: Simon and Schuster.

Seita, A. (1987). *Efumu Omurunyankole Rukiga, Omuhanda*. Mbarara.

Sokoloff, N. (1980). *Between Money and Love*. New York: Praeger. Tasnifu M.A Islamic University (Haijachapishwa).

Tumusiime, J. (1982). Entanda Yomugambi Worunyankole Rukiga. Kampala: Fountain Publishers.

Wafula, R. M. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*.Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wandera, S. P. (1996). *Usawiri wa Mwanamke Katika Ushairi wa Kiswahili 1800-1900: Uhalisia au Ugandamizaji? Tasnifu ya M.A, Chuo kikuu cha Egerton.63,66.*